



Issue no: 1 | Vol no: 6 | July 2025: 01-13

Uimarishaji wa Lugha za Kiasili Kupitia Vyombo vya Habari: Mfano wa Kinandi katika Runinga ya Kass

Melly Kipchirchir Joachim ⁽¹⁾ 
 Eric Walela Wamalwa ⁽²⁾ 
 Ernest Sangai Mohochi ⁽³⁾ 

Article History

Received: 2025-05-07
 Accepted: 2025-06-08
 Published: 2025-07-07

(1,2,3) Kibabii University, Kenya

Main author email: Mellyjoachim@gmail.com

Cite this article in APA

Melly, K. J., Wamalwa, E. W., & Mohochi, E. S. (2025). Uimarishaji wa lugha za kiasili kupitia vyombo vya habari: Mfano wa Kinandi katika Runinga ya Kass. *Editon consortium journal of kiswahili*, 6(1), 01-13. <https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v6i1.596>

Ikisiri

Lugha za kiasili ni muhimu sana katika kufanikisha mawasiliano kwa kuwa hutumiwa na watu wengi. Hata hivyo lugha hizi zinapitia changamoto kwa kuwa idadi ya wazungumzaji inazidi kupunguka. Hii ni kwa sababu lugha hizi zinapuuzwa huku lugha za Kiswahili na Kingereza zikitukuzwa. Hali hii inawafanya watu wengi kutumia Kiswahili katika mawasiliano ya mara kwa mara. Kutokana na umuhimu wa lugha za kiasili, ipo haja ya kuziimarisha. Makala hii inafafanua jinsi vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass vinachangia katika uimarishaji wa lugha ya Kinandi. Uchunguzi uliozaa makala hii ulifanyika katika kaunti ya Nandi. Uliongozwa na Nadharia ya Mawasiliano ya Sperka (1966). Washiriki 264 waliteuliwa kinasibu ili kuhusishwa katika uchunguzi. Mbinu za hojaji, utazamaji na mahojiano zilitumika katika kukusanya data. Data zilikusanywa kwa kutumia mwongozo wa utazamaji, hojaji na mwongozo wa maswali ya mahojiano. Data zilizokusanywa zilichanganuliwa kitakwimu na kimaelezo kwa kuzingatia lengo la utafiti kisha zikawasilishwa kwa kutumia asilimia na majedwali. Kutokana na uchunguzi huu, tumetambua kuwa lugha ya Kinandi inaweza kuimarishwa kupitia njia zifuatazo: Kuhimiza matumizi ya Kinandi katika mawasiliano ya mara kwa mara, kuwafundisha watoto kama lugha ya kwanza, kuifundisha shuleni kama mojawapo ya masomo, kuhimiza matumizi katika vyombo vya habari na kuhifadhi kwenye maandishi.

Maneno muhimu: Kilimo, kinandi, lugha, runinga, wakulima.



This article is distributed under the license of a [Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by-nc-sa/4.0/). It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

UTANGULIZI

Lugha za kiasili ni utambulisho wa makabila mbalimbali duniani na zina umuhimu mkubwa katika jamii, haya ni maelezo kwa mujibu wa UNESCO (2010). Hata hivyo lugha hizi zinakumbwa na changamoto tele zinazotishia utowekaji na ufifiaji wazo. Utandawazi umechangia ufifiaji wa matumizi ya lugha za kiasili. Kwa mujibu wa Kandagor na Toboso (2021), taarifa za tafiti zinazofanywa na wataalamu mbalimbali wa masuala ya lugha na utamaduni zinabainisha kuwepo kwa sababu mbali mbali zinazowafanya wazazi kutowafunza watoto lugha za kiasili. Moja ya sababu hizo ni dhana potovu iliyojengeka miongoni mwa jamii kuwa lugha za asili zinajenga ukabila. Nyingine ni ndoa za msetoa ambapo hata watoto wanaozaliwa vijijini wanalazimika kuzungumza Kiswahili wakati wote kama lugha ya mawasiliano.

Aidha mfumo wa maisha ya kisasa unaleta changamoto kubwa katika jitihada za kukuza lugha za kiasili, pamoja na kudumisha mila na desturi nzuri za makabila mbalimbali nchini. Matumizi ya teknolojia ya kisasa na mitandao ya kijamii yanaendelea kudidimiza matumizi ya lugha za kiasili (Misiko, 2018). Mawasiliano yote katika mitandao ambayo ni njia ya mawasiliano ya sasa yanatumia lugha ya Kiswahili na Kingereza huku lugha za kiasili zikipuuzwa. Ndoa za mseto, kukua kwa miji, maisha ya kuhamahama na kukua kwa mfumo wa elimu ni miongoni mwa sababu kubwa zinazodidimiza maendeleo ya lugha za kiasili. Tofauti na miaka ya nyuma ambapo ilikuwa nadra kuona watu wa makabila tofauti wakioana hivi sasa asilimia kubwa ya wanandoa ni watu wa makabila tofauti. Jambo hili linasababisha watoto kuzungumza lugha ya Kiswahili kama lugha yao ya kwanza.

Kutokana na maelezo haya, ni wazi kwamba lugha za kiasili zimeanza kukosa mvuto mbele ya kizazi kipyaa. Kizazi hiki hupendelea lugha za kigeni. Wazazi pia wamekuwa waumini wazuri wa kupoteza lugha zao za kiasili. Wazazi hawa wako radhi kuhakikisha kuwa watoto wao wanajifunza lugha ya Kingereza kama lugha ya kwanza wala si lugha za kiasili. Hali hii inabainisha umuhimu wa kuzipigania lugha hizi kupitia asasi mbali mbali. Makala hii inamulika hili kwa kuzingatia lugha ya Kinandi kupitia asasi ya vyombo vya habari hasa runinga ya Kass.

Wamalwa na Oluoch (2013), wanahoji kuwa lugha hufahamika kuwa katika hali hatari ya kuangamia kutokana na mambo yafuatayo: Ikiwa na wazungumzaji chini ya watu elfu tano, hali ya uwili lugha ambayo huwafanya wazungumzaji kupendelea lugha moja na kupuuzwa lugha nyingine, hali ya uchumi ya wazungumzaji wa lugha iliyo katika hatari huwafanya kupuuzwa lugha yao, mtazamo hasi kutoka kwa wazungumzaji wa lugha wanaoona lugha yao kuwa lugha isiyo na maana na kukosa kuwarithisha watoto lugha huifanya lugha kukosa kuendelezwa kwa vizazi vijavyo.

Naye Obiero (2010) akimnukuu crystal (2000), anasema kuwa kuna haja ya kuzihifadhi lugha za kiasili na kuzuia kuangamia kwa lugha hizi. Anasema kuwa, lugha za kiasili ni kitambulisho cha jamii inayoitumia. Vile vile lugha hizi ni nyenzo bora ya kuhifadhi historia ya jamii husika. Isitoshe, lugha ya kiasili hurahisisha mawasiliano kwa kuwa ni lugha ambayo hueleweka vyema baina ya watumiaji. Kwa hivyo lugha hizi zinapaswa kuimarishwa kimatumizi.

Katiba ya Kenya iliyoidhinishwa mwaka wa 2010 inahimiza makuzi ya lugha za kiasili. Hali hii inaonyesha kuwa matumizi ya lugha za kiasili yanapaswa kuhimizwa nchini. Sekta ya kilimo ni mojawapo ya ajenda kuu ya serikali ya sasa ya Kenya. Hii inadhihirika kutokana na mgao bora wa bajeti uliopewa sekta ya kilimo. Mgao huu unalenga kuhakikisha kuwa kuna utoshelevu wa chakula nchini na hivyo kupunguza gharama ya maisha. Kwa hivyo, kinyume na ilivyo sasa, kilimo ni eneo ambalo linahitaji matumizi mengi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari ili kuwafikia wananchi wengi zaidi mashinani ambao hujihusisha nalo.

Matumizi ya lugha za kiasili kupitisha habari kuhusu kilimo katika vyombo vya habari yatachangia pakubwa katika kustawisha kilimo kwani zinaweza kuwafikia watu wengi na kuwahamasisha kuhusu kilimo. Kutumiwa kwa lugha za kiasili katika vyombo vya habari kunahakikisha kuwa watu wengi wanapokea habari kuhusu kilimo kwa kina. Ingawa tafiti nyingi zimefanywa kuhusu lugha za kiasili na vyombo vya habari, mchango wa lugha ya Kinandi katika ustawi wa kilimo kupitia vyombo vya habari haujabainika wazi. Ni kwa msingi huu ndipo utafiti huu ulifanywa ili kuchunguza nafasi ya lugha ya

Kinandi katika ustawi wa kilimo katika jamii ya Nandi kupitia vipindi vya runinga ya Kass.

Utafiti huu ulichangia katika kutoa mielekeo ya uhifadhi wa lugha za kiasili hasa lugha mahususi ya Kinandi. Hapa, utafiti ulionyesha jinsi watangazaji huhimiza matumizi, uimarishaji na makuzi ya lugha ya Kinandi baina ya wanajamii. Isitoshe, ulitoa mwanga kuhusu majukumu yanayotekelezwa na lugha za kiasili nchini Kenya kupitia vyombo vya habari vinavyotangaza kwa lugha za kiasili. Katika hali hii utafiti huu ulitoa taswira kuhusu majukumu yanayotekelezwa na ya lugha ya Kinandi katika ustawi wa kilimo kupitia vipindi vya runinga ya Kass nchini Kenya. Aidha, ulitoa mapendekezo kwa wapangaji sera za lugha za kiasili nchini Kenya kuhusu ukuzaji wa lugha za kiasili na mchango ya lugha hizi katika ustawi wa kilimo. Hatimaye, tuna imani kuwa matokeo ya utafiti huu yalifaidi wizara ya kilimo katika kaunti ya Nandi. Hii ni kwa sababu matumizi ya lugha za kiasili katika vyombo vya habari kuwasilisha masuala ya kilimo yalileta athari chanya kwa wakulima wanaotazama vipindi vya kilimo.

Lengo kuu la utafiti lilikuwa ni kuchunguza jinsi vipindi vya kilimo huchangia katika uimarishaji wa lugha ya Kinandi. Ulihusisha kituo cha runinga cha Kass kinachotangaza kwa kutumia lugha ya Kinandi. Uteuzi wa runinga ya Kass ulitokana na kituo hiki kuwepo kwa zaidi ya miaka minane ikipeperusha matangazo na vipindi kwa lugha ya Kinandi. Kwa hivyo mtafiti alikadiria kuwa data toshelevu itapatikana. Vipindi vilivyohusishwa ni vipindi ambavyo vinahusu kilimo. Vipindi hivi ni: *Tugeet ab Kabotik* (Sauti ya mkulima), *Mungaret ak bandaptai* (Kilimo Biashara na maendeleo), *Baet ab Kiyakiik* (Ufugaji wa mifugo), *Minet ab bandek* (Upandaji wa mahindi), *Temisiet ab chaik* (Upandaji wa miche ya chai), *Boishonik ab Keljin* (Kazi zenye faida), *Mosoknatet eng Kabatisiet* (Teknolojia na kilimo), *Longet ab Kabotik* (Mkuki wa mkulima). Katika vipindi vilivyoteuliwa, mtafiti alilenga kuhakiki jinsi runinga ya kass huchangia katika uimarishaji wa lugha ya Kinandi kupitia vipindi vya kilimo. Vipindi vya saa tano usiku hadi saa moja asubuhi havikuhusishwa kwa kuwa ni vipindi vinavyolenga kuwaburudisha wanajamii tu.

Utafiti huu ulijikita katika runinga ya Kass ambayo hutangaza kwa lugha ya Kinandi. Wasikilizaji na watazamaji waliohusishwa katika utafiti ni wale ambao wana zaidi ya miaka kumi na minane. Isitoshe, wenye elimu na wasio na elimu walihusishwa kwa mizani sawa bila ubaguzi. Utafiti ulifanyika katika kaunti ndogo ya Emgwen iliyoko katika kaunti ya Nandi, nchini Kenya.

MAPITIO YA MAANDISHI

Hatari ya Kuangamia kwa Lugha za Kiasili

Kuangamia kwa lugha ni hali ambapo lugha iliyokuwa ikizungumzwa kwa wingi inajikuta katika hali ya kukosa wazungumzaji wake asilia. Hali hii hutokana na kupunguka kiidadi kutokana na vifo au wazungumzaji wake kuhamia lugha nyingine (Obuchi, 2019). Naye Obiero (2010), anaifasili dhana hii kuwa ni hali ambapo lugha inaweza kufa au kutoweka siku chache zinazokuja. Anazidi kusema kwamba lugha nyingi za kiasili zinaendelea kutawaliwa na lugha za Kiswahili na Kingereza, na katika mazingira haya, lugha hizi za kiasili zinapunguzwa kimatumizi na hivyo kuhatarishwa. Kwa mujibu wa Obuchi (2019) kuangamia kwa lugha kunasababishwa na mambo yafuatayo: Wasemaji wa lugha kusita kuizungumza, wasemaji kuizungumza katika miktadha finyu sana, Wasemaji kutumia sajili na mitindo michache ya lugha hiyo, Lugha kukosa kurithishwa kwa vizazi vinavyofuata na ikiwa wanaozungumza ni wazee pekee.

Mokaya (2020), anasema kuwa, lugha ya Kichina na ya Kimandarini ndizo zenye wasemaji wengi zaidi duniani. Kiingereza, licha ya kwamba kinasemwa kote duniani na pia ni lugha ya kimataifa ya kibiashara, ina wasemaji milioni 510. Izingatiwe kwamba Kiswahili kinasemwa na kufundishwa katika maeneo mengi duniani. Kwa sasa, idadi ya wazungumzaji wake inakisiwa kuwa zaidi ya milioni 200 duniani kote. Tukichukulia hii idadi, Kiswahili kitakuwa karibu nambari 10-15 miongoni mwa lugha maarufu duniani (Obuchi, 2019). Anazidi kuhoji kuwa, umaarufu wa Kiswahili unakifanya kuwa katika mstari wa mbele kuathiri au kuhatarisha lugha za kiasili katika eneo la Afrika Mashariki. Michieka (2012) anadai kwamba lugha huangamia kutokana na sababu zifuatazo:

Majanga

Majanga kama vile magonjwa yanaweza kuangamiza jamii nzima kiasi cha kuathiri hatima ya lugha. Kwa mfano, ikiwa wasemaji wa lugha maalumu ni wachache na ugonjwa kama vile Ebola uzuke, kuna uwezekano wa ugonjwa huu kuua idadi kubwa ya wasemaji. Ikiwa wasemaji watafariki, basi lugha iliyokuwa ikisemwa itakosa watu wa kuiendeleza na hivyo itakuwa hatarini. Sallabank (2010) anataja majanga mengine kama vile wimbi la tsunami, tetemeko la ardhi katika mataifa ya Asia kama vile Papua New Guinea na Visiwa vya Andamani. Majanga haya yana uwezo wa kuua jamii nzima pamoja na lugha yao.

Vita na Mauaji ya Halaiki

Michieka (2012) anasema kuwa vita na mauaji ya halaiki ni sababu moja kubwa sana inayoweza kutia lugha hatarini. Wakati wa mauaji ya halaiki, watu hutumia kigezo cha lugha kutenda maangamizi. Nchini Kenya, vita vya kisiasa (2007/2008) vilichukua mkondo wa kikabila. Ikiwa Mluo, Mluhya na Mkalenjini alipatikana katika mazingira ya Mgikuyu, aliangamizwa na vivyo hivyo, ikiwa Mkikuyu alijipata katika maeneo ya Mluo, Mkalenjini au Mluhya aliangamizwa (Obuchi, 2019). Hali hii ingawa ilichochea na madai ya wizi wa kura, mauaji hayakufuata chama bali kigezo kilikuwa lugha aliyozungumza mhusika. Baadhi ya manusura tuliowahoji walidai kwamba walikuwa wakiulizwa wazungumze lugha fulani, na endapo walishindwa, basi huo ndio ulikuwa mwanzo wa mateso yao.

Sallabank (2010) anatoa mifano halisi ya vita na mauaji ya halaiki yaliyowahi kutokea katika maeneo mbalimbali. Anasema kuwa, mauaji ya halaiki ya Tasmania yaliyoendelezwa na wakoloni yalipunguza idadi ya wazungumzaji wa lugha nchini humo. Vile vile Wabrazili asilia waliouawa kutokana na ung'ang'aniaji wa mashamba na rasilimali ulipingua idadi ya wazungumzaji wa lugha ya Kibrazili. Hatimaye mauaji ya Wayahudi zaidi ya milioni moja yalipunguza wazungumzaji wa lugha ya Kiyahudi. Mauaji haya yanadaiwa kuwa mauaji mabaya zaidi kuwahi kutokea kwa jamii inayozumza lugha moja.

Utawala wa Kiuchumi, Kiutamaduni na Kisiasa

Nettle na Romain (2000) wanadai kwamba kutawaliwa kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni

kulihatarisha lugha za Kikwechua na Kisorbia. Kwa mfano, Wasemaji wa Kimanchu walihamia Kichina wakati Ming alikuwa mfalme wa Beijing, China. Baada ya uvamizi wa Wamanchu, utawala huu mpya uliamuru Wamanchu wote kujifunza Kichina. Baada ya kuanguka kwa utawala huu wa Kimanchu, ilikuwa vigumu sana kwa Wamanchu kuanza tena kuzungumza lugha yao. Badala yake, wakaamua kuzungumza Kichina. Hatua hii ilipelekea kifo cha lugha ya Kimanchu. Obiero (2010) anadai kwamba humu nchini Kenya, Kisuba kilihatarishwa kiasi cha kukaribia kutoweka kwa sababu ya kutawaliwa kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni na jamii ya Waluo. Jamii ya Waluo ilikuwa kubwa mno kiasi cha kupelekea Wasuba kushindwa kujitenga nao. Kutawaliwa huku ndiko kulisababisha Wasuba kuhamia Kijaluo.

Utawala wa Kimabavu

Kutawaliwa kimabavu ni hali ambapo kundi moja kubwa na lenye nguvu nyingi hujilazimisha kwa kundi dogo na kuwapa masharti ya jinsi ya kuishi nao. Baadhi ya lugha ambazo zimeathiriwa na hali hii ni kama vile Kikurdi na lugha asilia za Marekani (Michieka, 2012). Naye Obiero (2010) anasema kuwa katika bara la Afrika, wakoloni waliwalazimishia Waafrika lugha zao za Kingereza, Kifaransa na Kireno na sera zao zililenga kuzibana lugha asilia. Walisisitiza kwamba lugha asilia hazikuwa na uwezo wa kuunganisha watu wote katika taifa. Kwa hivyo, lugha zilizokuwa bora zilikuwa za kikoloni. Nchini Kenya, Waingereza walipiga marufuku Kiswahili, na wakati mmoja wakasisitiza kwamba lugha asilia zifunzwe hadi darasa la tatu. Kingereza kilipewa nafasi kubwa licha ya kwamba palikosekana walimu wa kutosha wa kuifunza lugha hii. Hali hii iliathiri lugha za kiasili kwani wanafunzi walinyimwa nafasi ya kujifunza na kuzitumia lugha zao isipokuwa wakiwa nje ya shule.

Mielekeo Hasi

Mielekeo hasi huhusishwa na lugha za kiasili zisizokuwa na uwezo mkubwa. Lugha za kiasili huhusishwa na umaskini, ujinga wa kutojua kusoma na matatizo ya kijamii (Odero, 2013). Kwa upande mwingine, Odera (2013) anahoji kuwa lugha ya Kingereza na Kiswahili zinahusishwa na heshima kubwa, usomi wa hali ya juu, maendeleo kiuchumi na kukwepa umaskini. Mielekeo hii imeingizwa katika jamii zetu kiasi kwamba watu wengi

wanachukulia lugha za kiasili kama lugha ya watu wasiojua kusoma, maskini na wenye matatizo makubwa ya kijieleza kwa lugha ya Kingereza na Kiswahili. Mwelekeo kama huu unahatarisha lugha za kiasili. Kadiri mwelekeo hasi unavyozidi kujinyakulia nafasi kubwa katika jamii, ndivyo unasababisha wasemaji kuacha lugha zao na kuchukua lugha zinazodhaniwa kuwa bora.

Hali ya Maendeleo ya Miji

Maendeleo na ukuaji wa miji ni huathiri lugha za kiasili. Watu wanapogura kutoka vijijini na kuenda mijini, huenda wakakosa motisha na ilhamu ya kuzungumza lugha zao za kiasili. Hii ni kwa sababu miji ina wazungumzaji kutoka jamii (Obuchi, 2019). Ili watu hawa waelewane, huenda wakalazimika kuacha lugha zao za kiasili na kutumia lugha moja, pengine lugha ya taifa au rasmi. Hali hii inapoendelea kwa muda mrefu, wasemaji wa lugha mbalimbali huanza kusahau lugha zao. Wengi wao huweza kuoza kutoka jamii tofauti. Watoto wanaozaliwa hulazimika kujifunza Kiswahili. Kwa mantiki hii, watoto na vijana wengi wa mjini hawazifahamu wala kuzitumia lugha za kiasili.

Umuhimu wa Kuzihifadhi na Kuziimarisha Lugha za Kiasili

Lugha za kiasili katika mataifa mengi barani Afrika zimepuuzwa huku lugha za kigeni zikitukuzwa (Misiko, 2018). Ithibati ya hali hii hujitokeza bayana kupitia kwa sera za lugha zilizoibuka baada ya ukoloni. Sera hizi zilitukuza lugha za kigeni huku zikipuuzwa lugha za Kiafrika. Mataifa ya Afrika yanahitaji kuchukulia kwa umakini zaidi juhudi za kukuza lugha zao za kiasili na kuziinua hadi kiwango cha kuwa lugha za sayansi na uvumbuzi wa kiteknolojia (Mugambi, 2007). Akikubaliana na maoni haya, Misiko (2018), anasema kuwa, hali hii ya kuinua matumizi ya lugha za kiasili, hutokana na kuwepo haja ya kutumia lugha inayowawezesha waafrika kuelewa na kufanya maamuzi yanayohusiana na afya, kilimo, elimu, uraia, uchumi na pia mambo yanayohusiana na vipengele vingine vya kijamii. Lugha hizi za kiasili huenda zinaweza kuwafikia watu wengi haswa zikitumika katika vyombo vya habari.

Kamau (2015) anaonekana kuunga mkono umuhimu wa lugha za kiasili katika kuleta maendeleo ya kilimo katika jamii. Anasema kuwa, lugha za kiasili

huwa na umuhimu mkubwa katika jamii. Hii ni kwa sababu huibua hisia za uzalendo na mshikamano katika jamii na zaidi huwa hifadhi ya tamaduni za jamii mbalimbali na kuzipitisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Kamau (2015) ana msimamo kuwa, wakati jamii inapoipoteza lugha yao ya kiasili, huwa haipotezi tu nyenzo muhimu ya kuelezea, kuunda na kuhifadhi utamaduni wao bali hulazimika kujieleza na kuelezwa kupitia lugha na kumbukumbu za wageni. Kwa hivyo kulingana na Kamau (2015), kupoteza umilisi wa lugha ya kiasili ni sawa na kuipoteza utamaduni wako. Maoni haya ya Kamau (2015) yanathibitisha kuwa ipo haja ya kutafitia lugha za kiasili ili kuzihifadhi na kuendeleza matumizi yazo.

Kandagor na Toboso (2021), wakiangazia utandawazi kama tishio kwa lugha za Kiafrika, wanahoji kuwa, vyombo vya habari vina nafasi kubwa katika uhifadhi wa lugha. Kwa mujibu wa wataalamu hawa, matumizi ya lugha katika vyombo vya habari ni njia muhimu ya kuinua hadhi ya lugha. Vyombo vya habari huwa na usikilizaji mpana unaoweza kutumiwa kama njia ya kuwashirikisha watu katika mawasiliano yanayohusisha lugha za kiasili. Kandagor na Toboso (2021), wanadokeza kuwa, vyombo vya habari huwa na vipindi vya mazungumzo ya kidayolojia yanayoshirikisha mashabiki kupitia kwa simu.

Okombo (2014), anasema kuwa kupitia lugha za kiasili, tunaweza kueleza tamaduni zetu, ufahamu wetu kuhusu mimea yote, mkusanyiko wa wanyama na mkusanyiko wa maarifa tuliyonayo. Kwa hivyo, ni bayana kwamba lugha tunayotumia katika mazingira yetu ni muhimu sana. Anazidi kukariri kwamba Afrika inafaa ithamini na kukuza lugha za Kiafrika ili ziwe njia za muhimu zaidi za mawasiliano na za kujitambulisha kwa Waafrika wengi.

Misiko (2018), akishadidia umuhimu wa lugha za kiasili, anahoji kuwa hamna yeyote anayeweza kufikia ufanisi kwa kutumia lugha asiyoweza kuimudu kikamilifu. Anasema, watu huweza tu kuyaeleza na kuyafafanua mambo ya kimsingi katika utamaduni wao kwa kutumia lugha wanayomudu kikamilifu. Msomi huyu anahoji kuwa lugha hii aghalabu huwa ile ya kiasili. Naye Simala (2002), anatetea lugha za kiasili akisema kuwa, maendeleo

barani Afrika hayawezi kufikiwa bila lugha za kiasili kupata uwezo wa kuwasiliana. Uwezo huo hauwezi kufikiwa bila ya lugha za kiasili kuhusishwa kikamilifu katika uwasilishaji wa masuala muhimu yanayopatikana katika jamii husika. Kwa hivyo, iwapo lugha za kiasili zitahusishwa katika mawanda mapana ya mawasiliano, hadhi ya lugha hizo zitainuka na kuimarika

Ngugi (2014), anahimiza umuhimu wa kuthamini lugha za kiasili. Anasema kuwa fasihi ya Kiafrika kuandikwa kwa lugha za Ulaya tayari imestawi. Anauliza, mbona sasa tusianze kuzingatia lugha zetu za kiafrika? Msomi huyu anazidi kusema kwamba badala ya kuwepo mijadala kuhusu Kingereza, ambacho kinafanya vyema sana, wakati umefika tuekeze maarifa yetu, ubunifu, muda na pesa kwa lugha zetu za kiasili.

Kutokana mawazo haya ni dhahiri kwamba lugha za kiasili ni muhimu sana. Kwa hivyo lugha hizi zinapaswa kuhifadhiwa kwa kutumiwa katika mawasiliano ya mara kwa mara. Njia bora ya kuhakikisha kuwa lugha za kiasili zinatumiwa mara kwa mara ni kuzitumia katika vyombo vya habari vinavyowasilisha masuala kuhusu jamii. Hali hii itahakikisha kuwa lugha za kiasili zinazidi kuimarika. Ni katika msingi huu ndipo utafiti huu unafanywa ili kuchunguza jinsi vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass huchangia uimarishaji wa lugha ya Kinandi.

Misingi ya Kinadharia

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya mawasiliano ya Sperka (1966). Kwa mujibu wa nadharia hii, mawasiliano ni mchakato wa upitishaji ujumbe baina ya watu kwa kutumia lugha. Kwa hivyo tunaweza kusema mawasiliano ni ubadilishaji wa taarifa inayoleta maana baina ya pande mbili. Nadharia hii ina mihimili mitano. Mihimili hii ni kama ifuatayo: Uhamasishaji. Mhimili huu unasisitiza kwamba mawasiliano ni mchakato wa kuhamasisha taarifa kutoka kwa mtumaji hadi kwa mpokeaji. Katika muktadha huu, taarifa hutumwa na kupokelewa, na lengo ni kuhakikisha kwamba ujumbe unafika kwa usahihi kwa mpokeaji.

Maadili katika Mawasiliano. Mhimili huu unahusiana na matumizi ya mawasiliano kwa njia inayohusisha maadili na uaminifu. Unasisitiza

umuhimu wa kuzingatia uadilifu, haki, na heshima katika mawasiliano. Vilevile, unachunguza ni vipi mawasiliano yanaweza kuathiri haki za watu wengine na jamii kwa ujumla.

Mawasiliano ya Utamaduni. Mhimili huu unasema kwamba mawasiliano ni sehemu muhimu ya utamaduni na lina athari kubwa kwa jamii. unachunguza jinsi tamaduni, imani, na lugha ya jamii zinavyoshirikiana na jinsi zinavyoathiri mawasiliano.

Mawasiliano ya Kibinafsi. Mhimili huu unasisitiza umuhimu wa mawasiliano ya moja kwa moja kati ya watu wawili au zaidi. Hii inaangazia jinsi tunavyoshirikiana na kujenga uhusiano kupitia mazungumzo ya kibinafsi, na jinsi tunavyoshirikisha hisia na maoni katika mazingira ya karibu.

Mawasiliano ya Umma. Hii inahusiana na mawasiliano katika kiwango cha umma, ambapo watu wengi wanahusishwa katika mchakato wa mawasiliano. Inajadili jinsi vyombo vya habari, matangazo, na mikutano ya hadhara yanavyoweza kuathiri maoni ya umma na kushawishi jamii.

Utafiti ulizingatia mhimili wa kwanza, wa nne na wa tano. Mihimili hii ilisaidia utafiti huu kwa njia zifuatazo;

- i. *Uhamasishaji*. Mhimili huu ulisaidia kupima mchakato wa uhamishaji wa taarifa kutoka kwa mtumaji hadi kwa mpokeaji. Mtumaji ni mtangazaji wa vipindi vya kilimo huku mpokeaji akiwa mtazamaji wa vipindi hivi. Lengo la mhimili huu ni kuhakikisha kuwa taarifa ni sahihi na inapokelewa kwa njia rahisi. Lugha za kiasili huhakikisha kuwa taarifa inapokelewa kwa urahisi kwa kuwa inaeleweka vyema miongoni mwa watumiaji. Kwa hivyo lugha za kiasili zinapaswa kuendelezwa na kuimarishwa kimatumizi kupitia asasi za vyombo vya habari kwa kuwa huwafikia watu wengi. Mhimili huu ulisaidia kuchanganua data kuhusu jinsi vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass huimarisha lugha ya lugha ya Kinandi.
- ii. *Mawasiliano ya Utamaduni*. Kwa mujibu wa mhimili huu, utamaduni wa jamii haukamiliki bila lugha ya jamii hiyo.

Unasisitiza matumizi ya lugha za kiasili katika kufanikisha mawasiliano. Jamii inapotumia lugha yao ya kiasili, mawasiliano hufanikiwa zaidi. Kwa hivyo kuna haja ya kuimarisha matumizi ya lugha za kiasili kwa kubuni misamiati mipya na kusharabu maneno mengine ya lugha nyingine na kuyataifisha kuwa Kinandi. Kwa hivyo mhimili huu ulisaidia kuchanganua jinsi vipindi vya kilimo hubuni misamiati mipya na maneno mengine mapya ili kuhakikisha kuwa lugha ya Kinandi inaimarika

- iii. *Mawasiliano ya Umma*. Mhimili huu unajadili jinsi vyombo vya habari, matangazo, na mikutano ya hadhara yanavyoweza kuathiri maoni ya umma na kushawishi jamii haswa lugha za kiasili zinapotumika. Hii ina maana kuwa lugha za kiasili ni muhimu kwa kuwa zinapotumika katika vyombo vya habari vina uwezo mkubwa wa kuishawishi jamii. Kwa hivyo kuna haja ya kuzihifadhi, kuendeleza na kuimarisha matumizi ya lugha hizi kwa kubuni mikakati maalum. Mhimili huu ulisaidia utafiti huu kuchanganua data kuhusu jinsi runinga ya Kass imebuni mikakati ya kuendeleza na kuimarisha lugha ya Kinandi.

METHODOLOJIA

Mbinu zilizotumika katika utafiti huu ni kama zifuatazo: Hojaji, Utazamaji na usikilizaji wa vipindi na Mahojiano. Mbinu hizi zilitumiwa kukusanya data kwa kuzingatia lengo la utafiti. Data iliyokusanywa ilihusu jinsi runinga ya Kass huchangia katika uimarishaji wa lugha ya Kinandi kupitia vipindi vya kilimo. Utafiti huu ulizingatia mawaidha ya Sankoff (2001) na Saunders (2007) katika kuteua sampuli ya watazamaji wa runinga ya Kass. Watazamaji 264 waliteuliwa kinasibu ili kuhusishwa katika utafiti. Uteuzi huu uliongozwa na maoni ya Misiko (2018) kuwa asilimia 90 ya wazungumzaji wa lugha za kiasili hupatikana mashambani.

Hojaji zilitumiwa kuwapa watafitiwa uhuru wa kutoa maoni na mapendekezo yao. Ziliandaliwa kwa Kiswahili na Kinandi ili kuwafikia wale wasiomudu Kiswahili, na ziliwasilishwa moja kwa moja kwa

kwa watafitiwa ili kupunguza muda wa ukusanyaji wa data. Kabla ya kuwapa hojaji watafitiwa, mtafiti aliwaeleza watafitiwa lengo la utafiti na kuwahakikishia kwamba habari ambazo watatoa zitahifadhiwa kwa usiri wakati na baada ya utafiti. Maswali yalilenga jinsi vipindi vya kilimo vinavyochangia uimarishaji wa lugha ya Kinandi. Baada ya kugawanywa, miadi iliwekwa, na watafitiwa walipewa wiki mbili za kujaza hojaji. Mtafiti alizichukua mwenyewe, akizipitia ili kuhakikisha zimekamili, mbinu iliyosaidia kurekebisha dosari zozote, kama alivyosema Peil (1995).

Uchanganuzi wa yaliyomo ulihusisha kutazama vipindi vya kilimo vya runinga ya Kass. Vipindi hivi ni: *Tugeet ab Kabotik* (Sauti ya mkulima), *Mungaret ak Bandaptai* (Kilimo biashara na maendeleo), *Longeet ab Kabotik* (Mkuki wa mkulima), *Baet ab Kiyakiik* (Ufugaji bora wa mifugo), *Boishonik ab Keljin* (Kazi zenye faida), *Minet ab Bandek* (Upanzi wa mahindi), *Temisiet ab Chaik* (Upandaji wa Chai) na *Mosoknatet eng kabatisiet* (Teknolojia katika kilimo). Mwongozo wa uchanganuzi wa yaliyomo ulitumika kunakili yaliyomo katika vipindi hivi. Baada ya kubaini yaliyomo, data hii ilichanganuliwa ili kubaini jinsi vipindi hivi huleta ustawi wa kilimo miongoni mwa watazamaji. Mtafiti alirekodi vipindi kwa simu ya mkononi, akifuatilia nyakati za upeperushaji na kunasa simu za watazamaji, ambazo zilitoa data zaidi kuhusu jukumu la vipindi katika kuimarisha lugha ya Kinandi.

Mahojiano yalifanyika ili kupata maelezo zaidi ya majibu ya hojaji. Yalilenga watazamaji wa runinga ya Kass, hasa walioko mashambani, mahojiano yalitumia mwongozo uliowaruhusu watafitiwa kutoa majibu ya kina kuhusu uimarishaji wa lugha ya Kinandi kupitia vipindi vya kilimo. Majibu yalinakiliwa kwenye daftari na kurekodiwa kwa kinasa sauti cha simu kwa uchanganuzi wa data.

MATOKEO YA UTAFITI

Hatari ya Kuangamia kwa Lugha ya Kinandi

Kwa mujibu wa UNESCO (2010), lugha huangamia na kutoweka iwapo watumiaji wa lugha hiyo wataacha kuitumia. Wakati ambapo hakuna watumiaji wapya wa lugha husika, lugha hiyo huwa katika hatari. Kutokana na matumizi mapana ya lugha ya Kiswahili na Kingereza kama lugha kuu za

mawasiliano, lugha nyingi za kiasili ziko katika hatari ya kuangamia. Ni katika msingi huu ndipo mtafiti alilenga kupata maoni ya watazamaji kuhusu hatari ya lugha ya Kinandi kuangamia na kutoweka.

Watafitiwa walipewa kauli iliyowahitaji kutoa msimamo wao kuhusu kuangamia na kutoweka kwa lugha ya Kinandi. Matokeo yanawasilishwa katika jedwali lifuatalo;

Jedwali 1: Maoni ya Watazamaji kuhusu Kuangamia na Kutoweka kwa Lugha ya Kinandi

Maoni	Idadi	Asilimia
Nakubali	14	5.30
Nakubali kabisa	12	4.55
Sikubali Kabisa	145	54.92
Sikubali	59	22.35
Sina uhakika	34	12.88
Jumla	264	100

Kutokana na matokeo katika jedwali 1 asilimia 5.30 (N=14) ya watafitiwa walikubali kuwa lugha ya Kinandi iko katika hatari ya kuangamia huku asilimia 4.55 (N=12) wakikubali kabisa kuwa lugha hii iko katika hatari ya kuangamia na kutoweka. Aidha, asilimia 54.92 (N=145) hawakukubali kabisa kuwa lugha ya Kinandi iko katika hatari ya kuangamia. Hii inadhihirisha kuwa wazungumzaji wa Kinandi wanapenda lugha yao na wanasisitiza matumizi yake katika mawasiliano. Ikiwa Kinandi msisitizo huu ina maana kuwa jamii ya Nandi inauenzi utamaduni wao kama unavyoelekeza nadharia ya mawasiliano ya Sperka (1966) utamaduni wa jamii hautakamilika bila lugha ya jamii hiyo.

Isitoshe, asilimia 22.35 (N=59) hawakukubali kuwa lugha hii iko katika hatari ya kuangamia. Hatimaye, asilimia 12.88 (N=34) hawakuwa na uhakika kuhusu kuangamia au kutoweka kwa lugha hii. Matokeo

haya yanaonyesha kuwa wakaazi wa kaunti ya Nandi wana imani na matumizi ya lugha ya Kinandi na hawakubali kutoweka na kuangamia kwa lugha hii hata baada ya Mokaya (2020) kusesitiza kuwa lugha za kiasili kwa ujumla zinapuuuzwa kimatumizi.

Mbinu za Uimarishaji wa Lugha ya Kinandi

Orao (2012) anahoji kuwa kuna haja ya kuziifadhi lugha za kiasili na kuzuia utowekaji wazo. Anaendelea kusema kuwa kuna mbinu anuwai zinazoweza kutumiwa kuziifadhi kulingana na watumiaji wa lugha katika jamii husika. Hii ndiyo sababu mtafiti alilenga kubaini mbinu ambazo zinaweza kutumika ili kuendeleza na kuimarisha lugha ya Kinandi na hivyo kuzuia dhidi ya kuangamia na kutoweka. Watafitiwa waliombwa kutoa maoni kuhusu mbinu zinazoweza kutumiwa ili kuimarisha na kuendeleza matumizi ya lugha ya Kinandi. Matokeo yanawasilishwa katika jedwali lifuatalo;

Jedwali 2: Mbinu za Uimarishaji wa Lugha ya Kinandi

Mbinu	Idadi	Asilimia
Kuhimiza matumizi katika mawasiliano ya kila mara	169	64.02
Kuwafundisha watoto kama lugha ya kwanza	139	52.65
Kufundisha shuleni kama mojawapo ya masomo	98	37.12
Kutumika zaidi katika vyombo vya habari	231	87.50
Kuhifadhi kwenye maandishi	67	25.39
Kutumia katika mitandao ya kijamii	92	34.85
Kuandika majarida ya Kinandi	84	31.82
Kufanya utafiti zaidi katika Kinandi	78	29.55
Jumla	264	100

Kwa mujibu wa matokeo katika jedwali 2, asilimia 64.02 (N=169) ya watafiti walihoji kuwa ili kuimarisha lugha ya Kinandi, matumizi yake yanapaswa kuhimizwa katika mawasiliano ya kila mara. Mawasiliano haya yatafanikishwa kwa sababu lugha ya Kinandi inaeleweka vyema miongoni mwa watumiaji kama anavyodahili Sperka (1966) katika nadharia ya mawasiliano. Lugha za kiasili huhakikisha kuwa taarifa inapokelewa kwa urahisi kwa kuwa inaeleweka vyema miongoni mwa watumiaji.

Walela na Oluoch (2013) wanahoji kuwa mbinu mojawapo wa kuhifadhi na kuendeleza lugha za kiasili ni kuwarithisha watoto ili kuhakikisha kuwa lugha inapitishwa kutoka kiazazi kimoja hadi kingine. Asilimia 52.65 (N=139) walishadidi maelezo haya kuhusu uhifadhi wa lugha ya Kinandi. Aidha, asilimia 37.12 (N=98) walikubali kuwa lugha ya Kinandi inapaswa kufundishwa shuleni kama mojawapo ya masomo. Wakati huo huo asilimia 87.50 (N=231) walisema kuwa lugha hii inapaswa kutumika zaidi katika vyombo vya habari. Asilimia 25.39 (N=67) walikuwa na wazo kuwa lugha ya Kinandi iweze kuhifadhiwa kwenye maandishi. Kando na hayo, asilimia 34.85 (N=92) walihoji kuwa lugha Kinandi inaweza kuimarika ikiwa itatumika katika mitandao ya kijamii huku asilimia 31.82 (N=84) wakipendekeza uandishi wa majarida ya Kinandi kama njia mojawapo ya kuimarisha Kinandi. Hatimaye asilimia 29.55 (N=78) wakisema kuwa

tafiti zaidi zinapaswa kufanywa kwa lugha ya Kinandi.

Matokeo haya yanashadidia ugunduzi wa Musau (2012) kwamba ili kusaidia kueneza matumizi ya lugha za kiasili, vyombo vya habari vinafaa kutumika katika kueneza matumizi yazo. Anapendekeza kuwa ili kueneza matumizi ya lugha za kiasili, serikali ya Kenya inapaswa kubuni sera zinazohitaji kila chombo cha habari kutenga asilimia fulani ya utangazaji wake kuwa utangazaji kwa kutumia lugha za kiasili. Hata hivyo maoni haya ya Musau (2012) ni kinyume na alivyogundua Misiko (2018) kwamba serikali ya Kenya haiungi mkono lugha za kiasili kama njia ya kupasha habari kwa umma kwa hofu ya kusababisha tofauti za kikabila.

Mchango wa Vipindi vya Kilimo katika Uimarishaji wa Lugha ya Kinandi

Kwa mujibu wa Kandagor na Toboso (2021), vyombo vya habari vina nafasi kubwa katika uimarishaji na uendelezaji wa lugha. Vyombo hivi huwa na usikilizaji mpana unaoweza kutumiwa kama njia muhimu ya kuinua hadhi ya lugha. Kwa kuzingatia mdokezo huu wa Kandagor na Toboso (2021), mtafiti alilenga kubaini mchango wa vipindi vya kilimo katika kuimarisha lugha ya Kinandi. Kwa hivyo watafiwa waliulizwa jinsi vipindi vya kilimo vinachangia katika kuimarisha lugha ya Kinandi. Matokeo yanawasilishwa katika jedwali lifua

Jedwali 3: Mchango wa Vipindi vya Kilimo katika Uimarishaji wa Lugha ya Kinandi

Mchango	Idadi	Asilimia
Kupatikana kwa misamiati mipya	58	21.97
Matumizi ya Kinandi mara kwa mara katika vipindi	216	81.82
Watangazaji wanahimiza matumizi ya Kinandi	189	71.59
Watazamaji wanaonea fahari matumizi ya Kinandi	145	54.92
Matumizi ya Kinandi hayasaidii chochote	4	1.52
Sina Uhakika	3	1.14
Jumla	264	100

Kwa mujibu wa matokeo katika jedwali 3, matokeo yalibaini kuwa vipindi vya kilimo huimarisha lugha ya Kinandi kwa kuzua misamiati mipya ya lugha hii. Hii iliwakilishwa na asilimia 21.97 (N=58). Watafitiwa hawa walikiri kuwa kuna misamiati mipya inayozuka kutokana na vipindi vya kilimo. Misamiati hii ni kama ifuatayo;

- i. *Chesogit'* - inayomaanisha aina bora ya majani chai iliyoanzishwa hivi majuzi.
- ii. *Cheborosinik* – Mahindi inayokua baada ya miezi mitatu.
- iii. *Tundubaru* – Eneo la kukusanya majani chai kabla ya kupelekwa kwenye kampuni.

Kuna misamiati vile vile iliyopatikana kwa kusharubu maneno kutoka lugha Kingereza na kuyataifisha kwa kutumia fonolojia ya Kinandi. Maneno hayo ni kama yafuatayo;

- i. *Teri* – Neno hili lilipatikana kwa kukopwa kutoka neno la Kingereza (Dairy). Humaanisha chumba cha kuwalisha ngombe.
- ii. *Tipit* – Neno hili lilikopwa kutoka Kingereza (Dip). Humaanisha chumba cha kuwanyunyizia mifugo dawa ya kuua kupe.
- iii. *Topa* – Neno lilikopwa kutoka Kingereza (Dopper). Humaanisha aina ya kondoo wa kisasa.

Asilimia kubwa zaidi ya 81.82 (N=216) ilishadidia wazo kuwa matumizi ya mara kwa mara ya lugha ya kinandi kuwasilisha vipindi vya kilimo huchangia

katika kuimarisha lugha hii. Matumizi ya mara ya lugha ina maana kuwa kuna mtazamo chanya kuihusu kwa watumiaji. Mtazamo chanya utahakikisha kuwa Kinandi kinarithishwa kwa watoto ili kiendelezwe na kuimarishwa. Hali hii inashididiwa na nadharia ya Mawasiliano ya Sperka (1966) kuwa lugha inayotumika mara kwa mara katika mawasiliano huimarika.

Hata hivyo, matumizi haya ya mara kwa mara yalipingwa awali na shirika la utangazaji la Uingereza (BBC) mwaka 2008. Shirika hili lilidai kwamba vyombo vya habari vinavyotangaza kwa lugha za kiasili vilitumika kueneza chuki za kikabila mwaka 2006 kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2007. Kwa hivyo, shirika hili lilipendekeza kuwa lugha za kiasili katika vyombo vya habari zisitumike mara kwa mara. Hata hivyo, Kinoti (2021) anayapinga madai haya anaposema kuwa vyombo vya habari vinavyotumia lugha za kiasili ni muhimu sana na vinapaswa kuhimizwa hasa mashambani ambako kuna maendeleo ya kilimo.

Vile vile, asilimia 71.59 (N=189) ya watazamaji walihoji kuwa watangazaji wanahimiza matumizi ya Kinandi katika matangazo yao ya vipindi vya kilimo. Watangazaji wa vipindi vya kilimo waliwahimiza watazamaji kutumia Kinandi wanapopiga simu wakati wa majadiliano ya kilimo. Vile vile watangazaji hawa waliwamiza watazamaji kutumia Kinandi wakati wa mawasiliano ya kawaida wakiwa katika shughuli zao za kilimo. Kwa mujibu wa nadharia ya Mawasiliano yake Sperka (1966) lugha

inayotumiwa katika kiwango cha umma, ambapo watu wengi wanahusishwa katika mchakato wa mawasiliano, huimarisha lugha husika. Kwa hivyo, Kuhimiza matumizi ya Kinandi kulisaidia kuimarisha lugha hii.

Aidha, watazamaji walionea fahari matumizi ya lugha ya Kinandi katika kuwasilisha vipindi vya kilimo. Fahari ya lugha za kiasili zinatiliwa maanani na Mokaya (2020) ambaye anasema kuwa lugha za kiasili ni fahari kwa taifa la Kenya kwani kuwepo kwa lugha mbali mbali katika taifa moja ni sababu tosha kwa taifa kujivunia. Hii ikiwa asilimia 54.92 (N=145). Kuionea fahari lugha ya Kinandi kuliwafanya watazamaji waweze kuitumia lugha hii bila kuogopa na hivyo kuendeleza matumizi yake. Asilimia 1.52 (N=4) walisema kuwa matumizi ya Kinandi hayasaidii chochote huku asilimia 1.14 (N=3) wakikosa kuwa na uhakika kuhusu matumizi ya lugha ya Kinandi katika runinga ya Kass.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Utafiti huu ulilenga kubaini mchango wa vipindi vya kilimo katika runinga ya Kass katika kuimarisha lugha ya Kinandi. Kwanza ulitaka kupata maoni ya watazamaji wa runinga ya Kass kuhusu kuangamia na kutoweka kwa lugha ya Kinandi. Asilimia 54.92 (N=145) ya watafitiwa hawakukubali kabisa kuwa lugha ya Kinandi iko katika hatari ya kuangamia. Hii ina maana kuwa lugha ya Kinandi iko imara katika matumizi yake kufanikisha mawasiliano. Matokeo haya yanathibitisha kuwa lugha ya hii inapaswa kuimarishwa na kuendelezwa kimatumizi.

Kuhusu mbinu za uimarishaji wa lugha ya Kinandi, watafitiwa walikiri kuwa njia mwaka ya kuimarisha lugha ya Kinandi ni kuhimiza matumizi yake katika vyombo vya habari. Hii ikiwa asilimia 87.50 (N=231). Isitoshe ilibainika kuwa matumizi ya mara kwa mara ya Kinandi katika kuwasilisha vipindi vya kilimo kulisaidia kuimarisha lugha hii. Asilimia 81.82 (N=216) ya watafitiwa ilishadidia uimarishaji wa Kinandi katika hali hii ya matumizi. Matumizi zaidi ya lugha hii yanapaswa kuhimiza ili iendeleo kuimarika. Wazazi wanapaswa kuwafundisha watoto wao lugha ya Kinandi kama lugha yao ya kwanza. Hali hii itahakikisha kuwa lugha ya Kinandi inarithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

Makala haya yanathibitisha kuwa lugha za kiasili zina umuhimu mkubwa na zinapaswa kuhifadhiwa, kuimarishwa na kuendelezwa kimatumizi. Serikali za kaunti zinapaswa kubuni mikakati ya kuhakikisha kuwa lugha za kiasili zinahimizwa kimatumizi. Viongozi wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kuendeleza matumizi ya lugha za kiasili. Vyombo vya habari vinavyotangaza kwa lugha za kiasili vinapaswa kuhimiza matumizi yazo kwa wasikilizaji na watazamaji. Hali hii itahakikisha kuwa kuna mtazamo chanya wa matumizi ya lugha za kiasili katika mawasiliano ya mara kwa mara.

Mapendekezo: Uchunguzi huu unapendekeza kuwa ili kuimarisha zaidi lugha ya Kinandi, vipindi vya kilimo vinapaswa kuwahusisha vijana kwa kiwango kikubwa ili kuhakikisha kuwa wanabadili mielekeo hasi kuhusu matumizi ya Kinandi. Runginga ya Kass inapaswa kubuni vipindi zaidi vya mara kwa mara vinavyowahusisha vijana kwa kiwango kikubwa.

Aidha, unapendekeza kuwa uwasilishaji wa vipindi vya kilimo uhusishe zaidi teknolojia ya habari na mawasiliano ili kuhakikisha kuwa uwasilishaji wa vipindi hivi unafanywa kwa njia ya kisasa.

Isitoshe, pendekezo linatolewa kwa runinga ya Kass kubuni sera zinazoongoza matumizi ya kinandi katika kuwasilisha vipindi vya kilimo. Sera hizi zitahakikisha kuwa matumizi ya Kinandi yanaongozwa na sera maalum.

Kando na hilo runinga ya Kass ya inapendekezewa kuanzisha vipindi vinavyolenga kuwaelimisha wanandi lugha ya Kinandi. Kwa kufanya hivi lugha ya Kinandi itaimarika zaidi kwa kuwa wanaomudu Kinandi wataongezeka kutokana na mafunzo haya.

Hatimaye, runinga ya Kass inapendekezewa kuandaa misafara ya barabarani inayohusisha utangamano na wananchi ili kuwahimiza kusikiliza vipindi vyao vya kilimo na kuwahimiza kutumia lugha ya Kinandi katika mawasiliano ya mara kwa mara baina yao. Kwa kufanya hivi umaarufu wa Kinandi utashuhudiwa kama lugha ya mawasiliano. Umaarufu huu utaimarisha matumizi ya Kinandi na hivyo kuitoa katika hatari ya kuangamia.

MAREJELEO

- Ary, D. (1972). *Introduction to research in education*. New York: Holtrine.
- Creswell, J. (2014). *Research design*. London: Sage Publishers.
- Crystal, D. (2000). *Language death*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Enon, C. (1998). *Education research and measurement*. Kampala: Makerere University Publishers.
- Kamau, M. (2015). *Vernacular radio and democracy in Kenya: A historical reconstruction of audiences' usage of Kass and Inooro Radio stations in Uasin Gishu District* (Unpublished master's thesis). Moi University.
- Kandagor, M., & Toboso, M. (2021). Utandawazi kama tishio kwa lugha za Kiafrika. Katika Mauka, L., Jebet, A., & Kyeu, D. (Wah.), *Jarida la Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika*, Chuo Kikuu cha Moi (kur. 70–75).
- Kinoti, W. (2021). *Mchango wa lugha za kiasili katika ufikiwaji wa maendeleo endelevu*. Embu: East Africa Scholars Publishers.
- Michieka, P. (2012). *African languages, literatures and postcolonial modernity*. Cambridge: Cambridge University Publishers.
- Misiko, W. (2018). *Lugha kama rasilmali ya jamii: Uchunhuzi wa redio za FM zibazotumia Kibukusu katika Kaunti ya Bungoma* (Tasnifu ya Uzamifu, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Moi.
- Mokaya, M. (2020). *Language policy and practices in education in Kenya and Uganda: Perception of parents, pupils and teacher on the use of mother tongue*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Mugambi, B. M. (2007). Rural development in Kenya: Is Kiswahili the language of hope or despair? Katika Shitemi, N. L., Noordin, M., Opijah, A., & Mukuria, D. (Wh.), *Kiswahili a tool for development, the multidisciplinary approach* (uk. 124–132). Eldoret: Moi University Press.
- Mugenda, O., & Mugenda, A. (2003). *Research methods, qualitative & quantitative approaches*. Nairobi: Acts Press.
- Musau, P. (2012). The development of African languages for modern discourse: The case of Kiswahili. Katika Owino, R. F. (Mh.), *Speaking African: African language for education and development* (uk. 253–265). Cape Town: CASAS.
- Nettle, D., & Romain, S. (2000). *Vanishing voices: The extinction of the world's languages*. Cambridge: Cambridge Publishers.
- Ngugi, G. (2014). *Radio listening habits among rural audiences: An ethnographic study of Kieni West Division in Central Kenya* (Tasnifu ya Uzamifu). The Strips College of Communication of Ohio University.
- Obuchi, S. (2019). *Juhudi za kukabiliana na kuangamia kwa lugha za Kiafrika*. Moi University Press.
- Obiero, J. (2010). From assessing language endangerment or vitality to creating and evaluating language revitalization programs. *Nordic Journal of African Studies*, 19(4), 201–226.
- Odera, F. (2013). *School radio programmes: A case study of its use in selected institutions in Nyanza Region in Kenya*. Great Britain: Wales Publishers.
- Okombo, O. (2014, April 12). Languages hold the key to Kenya's economy. *The Saturday Nation*, uk. 21.
- Orao, J. (2012). *The Kenyan indigenous languages and the mass media: Challenges and opportunities*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Editon Consortium Journal of Kiswahili

- Peil, M. (1995). *Social sciences research methods: A handbook for Africa* (2nd rev. ed.). Nairobi: East African Educational Publishers.
- Sankoff, D. (2001). Statistics in sociolinguistics. Katika Mestchire, R. (Ed.), *Concise encyclopedia of sociolinguistics* (uk. 828–834). Elsevier B.V.
- Sallabank, J. (2010). *Language endangerment: Problems and solutions*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Saunders, P. (2007). *Approaches to social research*. New York: Oxford University Press.
- Simala, I. (2002). Empowering indigenous African languages for sustainable development. Katika Owino, R. (Mh.), *Speaking African: African language for education and development* (uk. 45–53). Cape Town: CASAS.
- Sperka, N. (1966). *Communication theory*. New Delhi: Sterling Publishers.
- UNESCO. (2010). *Why and how Africa should invest in African languages and multilingual education: An evidence and practical based advocacy brief*. Hamburg: UNESCO Institute of Longlife Learning.
- Walela, E. W., & Oluch, B. (2013). Language endangerment and language maintenance: Can endangered indigenous languages be electronically preserved? *International Journal of Humanities and Social Sciences*, 3(7).